

PAZA SAUTI

Sehemu ya Harakati ya Ngeti



**HAKI YA
KUWA
BINTI**

Simulizi ya mabinti kupingana na ukatili wa kijinsia

Simulizi za Harakati za Ngeti
Paza Sauti - *Haki ya Kuwa Msichana*

Kimetayarishwa na: Tai Tanzania
S.L.P. 54631
Kinondoni, Dar es Salaam


Kimefadhiliwa na: Mundo Cooperante


Kimeandikwa na: Padili James
Msanifu: Gwamaka Mwabuka
Wachoraji: Chris Katembo na Yohana Mwenda

"Paza Sauti," hadithi inayojenga ndani ya ulimwengu wa kusisimua wa Simulizi za Harakati za Ngeti, ikiletwa kwako na Tai Tanzania. Kama shirika linalofanya kazi ya kusimamia haki za wasichana nchini Tanzania kupitia ubunifu, wanachunguza changamoto wanazokabiliana nazo wasichana—kama vile upatikanaji mdogo wa elimu na afya, ndoa na ujauzito wa mapema, na kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia. Kupitia ukusanyaji wa takwimu, Tai inasimulia hadithi zenye kuvutia kwenye muundo wa filamu za vikaragosi, vitabu vya michoro, na matangazo ya redio kwenye majukwaa ya jadi na dijitali.



KATIKA MJI MDOGO WA MZINGA, MABINTI WAMEKUA WAKIPATA UJAUZITO, NA KUPITIA CHANGAMOTO ZA USHAWISHI WA NGONO TOKA KWA VIJANA HASA WAENDESHA BODABODA. WAMEKUWA WAKIPITIA UKATILI WA KIJINSIA NA KUKATISHA MASOMO YAO.





SASA MCHUMBA
JIONI NIKUPITIE,
TWENDE UKALE CHIPS,
ALAFU TUKAANGALIE
MUVI GETO EEEH!?


AHSANTE!
ILA MI NAOGOPA
BWANA.

LUNAOGOPA NINI
MTOTO MZURI HIVI EEH!?
ACHA UOGA UVUUNE
ASALI.



WE SOFI,
SI NILIKWAMBIA!?
ANA LAKE HUUYU.




BEBI SOFI.
KAMA LUNAONA UCHOYO,
MWALIKE NA MWENZIO.
EEH SAWA!?



NASHUKURU,
ILA HAPANA.
TUWE MARAFIKI TU.



NGETI NA SOFI WAPO KIDATO CHA PILI, NGETI ALIFANYA VIZURI DARASANI, LAKINI SOFI ALIKUWA ANAMATOKEA YA KUFELI. MWALIMU WA ZAMU ALIPOWAONA WANAFIKA WAMECHELEWA AKATUMIA FURSA HIYO KUTUMIA FIMBO KUGUSA KIFUA CHA NGETI KUMAANISHA KUWAONYA.



NGETI HAKUWA BINTI MWENYE UOGA, ILA UKIMYA WA WENZAKE UMEMFANYA KUWA DHAIFU KIFIKRA NA USHUJAA WAKE UNAFIFIA.

HIVI KWANINI ANIGUSE KIFUANI NA FIMBO? HII SIO SAWA. WEWE UNAONA NI SAWA?

EH, TUFANYAJE? HAKUNA WA KUTUSIKILIZA RAFIKI YANGU.

KWANINI ANIGUSE MATITI?! AU NIMEKOSEA? SIJUI NIKASEME WAPI!.



AHSANTE, MAMA SOLO.

MUDA WA MAPUMZIKO, WAKATI NGETI NA SOFI WANATAKA KULA, FAKI AKAWASHITUA KIBABE,

OYA!

HAHAA! MADEM WAOGA! MMESHTUKA MPAKA MMETUPA MSOSI.

MIMI KIRANJA WA MICHEZO, MWALIMU HANIFANYI CHOCHOTE. OYA, NAOMBA JIBU LANGU BASI! EH?

NITAKUPATA TU, SUBIRI.

AGH! FAKI, MCHOKOZI! NA NITAENDA KUKUSEMELEA KWA MWALIMU

NAOMBA UNIACHE SITAKI MAHUSIANO, NIACHE NISOME.

AKIWA NYUMBANI NGETI ALILELEWA NA BABA YAKE AMBAYE ALIPATA WAKATI MGUMU KUONGEA NAE KUHUSU MAMBO YANAYOMSIBU KAMA BINTI.



MZEE JAMBE
ATAKUPA MAISHA
MAZURI, NA UKIWA
UMEKEKETWA...

BIBI NA MAMA SOFI WALIONA JINSI SOFI HAFANYI VIZURI SHULENI, HIYO IKAWA SABABU YA KUMUOZESHA KWA MZEE JAMBE.



UACHE UBISHI,
SHULE IMESHA KUSHINDA
NI MUDA UOLEWE!



BIBI, MIMI
SITAKI KUOLEWA.
NAOGOPA KUKEKETWA.
SITAKI KUFA BIBI!



ACHA UJINGA!
LAZIMA UKEKETWE NA
UOLEWE, TUPUNGUZE
MIZIGO KWENYE
UKOO.



ENDELEA KUOGA
VIZURI, KUJIREMBA,
WAOAJI WANAKUJA
JUMAMOSI


KWA UPANDE WA NGETI ALIENDELEA KUPATA VISHAWISHI VINGI ALIPOKUWA NYUMBANI AKIMSATIDIA BABA YAKE.



BIBIE NGETI
NIMEKUJA TENA!
JIBU LANGU
UMELIANDAA.



FAKI NIACHE
KAMA UNATAKA
SAMAKI, NUNUA
UONDOKA.



NGETI ALIMSIMULIA MWALIMU MAUA KILA KITU KILICHOTOKEA HASA UKATILI WA KIJINSIA, UONEVU NA MASWAIBU YAKE. MWALIMU MAUA HAKUWA NA JINSI BALI KUMBADILI MTAZAMO KABISA.

MWALIMU HAYO NDIYO MATENDO TUNAYO PITIA KILA SIKU!

NGETI NI VIZURI UMEKUWA NA UJASIRI WA KUZUNGUMZA. NATAKA KUKUPA VITABU VIWILI....



PAZA SAUTI, USIOGOPE, TOA TAARIFA, UKIMYA NI HATARI ZAIDI. HAYA, SHIKA HIVI..




LIFANYE KAMA NILIVYO KWAMBIA NA USIHOFU KUHUSU MWALIMU DILITI NITALIFANYIA KAZI.

NGETI ALIFUNGUKA AKILI, NI KAMA VILE ALIKOSA MSUKUMO MDOGO TU, AMBAO MWALIMU MAUA, AMEMPATIA. NGETI HARUDI NYUMA.



NITAANZA KUONGEA NA BABA, NI MUHIMU AELEWE MAMBO YANAYOENDELEA KWENYE DUNIA YANGU KAMA BINTI.





1. JE UNAELEWA UKATILI WA KIJINSIA NI NINI? TUELEZEE MAANA YAKE.
2. JE UNAZIFAHAMU AINA MBALIMBALI ZA UKATILI WA KIJINSIA? ZITAJE.
3. JE NI SAWA KWA MWALIMU WA ZAMU KUMSHIKA SHIKA KIFUANI NGETI NA FIMBO YAKE, KWA SABABU YA KUCHELEWA DARASANI?
KAMA JIBU LAKO NI NDIO AU HAPANA, TOA SABABU.
4. JE WEWE KAMA BINTI UNaweza KUFANYA NINI KUONDOKANA NA UKATILI WA KIJINSIA UNAOFANYIKA MASHULENI? TUELEZEE KWA KINA.

12:39 ALFAJIRI. SHULE YA SEKONDARI BUMBUI





MWAMBIE
MWALIMU MAUA,
MIMI AMENISAIDIA VIZURI
MNO SOFI.

HEBU NIACHE TU,
NIFANYE MAAMUZI
YANGU MWENYEWWE.

NGETI ALIPIGA MOYO KONDE NA KUANZA
CHUKUA HATUA NEUMU AMBAZO HAKUWAHI
ZIFIKIRIA ILI KUSOMA KWA AMANI NA
KUISHI KAMA BINTI ANAYETAKA TIMIZA
NDOO ZAKE.

AKINIELEWA VIBAYA
ITAKUWAJE...NA...
MMH. NGOJA TU
NISEME...



KUNA KITU NATAKA...
NI..KWAMBIE, NIMEKUWA
NACHO KWA MUDA MREFU,
KINA NISUMBUA.

KITU?!
KINAKUSUMBUA?!



NINI NGETI?
KAMA UNAMAWAZO
UNAWAZA NINI
MWANANGU!?



CHOPA ALIKUWA MWANAUME WA TAMADUNI, HAKUWA NA UTASHI WA KUELEWA MALEZI
MAMBO LEO NA KITENDO CHA BINTI YAKE KUFUNGUKA, KILIMSTUA.



EH, HUJAWAHI
KUSISITIZA HIVI, NAONA
TUWEKE MIZIGO CHINI
NIAMBIE MWANANGU

LINAJUA BABA,
KWA MIEZI!....

BAADA YA KUJUA KINACHOENDELEA KATIKA MAISHA YA BINTI YAKE, CHOPA, ALIYEKUWA NA MITAZAMO YA KALE, ALIKUWA TAYARI KUIVUNJA KUMLINDA BINTI YAKE.



CHOPA ANASIKITIKA NA KUMKUMBATIA NGETI KWA UCHUNGU.




...NDIO HIVYO!
YAANI NILIOGOPA
KUKWAMBIA, MAANA
SIKUJUA UTAFIKIRIA
NINI!

AAAH MWANANGU.
NDIO UMEPITIA YOTE HAYA
..AAAAAAH. USILIE MWANANGU,
USIJALI NITAKULINDA.




BAADAJE JIONI: SOFI HAKUWA NA MTU WA KUMTETEWA. SOFI ALIKUWA PEKE YAKE NA ZINJA - ALIONA UPENYO PEKEE WA KUFANYA MIPANGO YAKE.



AH!, BIBI YAKO MCHAWI!
ANAKUOZESHAJE, WAKATI WEWE
NI WANGU EEH. NITAKULINDA,
NITAKUHUDUMIA USIHOFU.

KWELI ZINJA,
UNAMANISHA UNAYOSEMA.
SINA WA KUNISAIDIA.
USINIDANGANYE ZINJA.

LONGO NILISHA
ACHA KABISA SOFI.
USIJALI.SASA
FANYA HIVI...



KIJIJI CHA BUMBUI



CHOPA ALIKUWA MWANAUME MWENYE HESHIMA
KIJIJINI NA NENO LAKE LILISIKILIZWA KWA UMAKINI.



MWENYEKITI,
NAOMBA UCHUKUE HATUA
UKATI WA KIJINSIA
UNAWA ATHIRI SANA
MABINTI.

NAKUAHIDI CHOPA
HILI SUALA LAZIMA
TULIFANYIE KAZI!. NITAANZA
NA UCHUNGUZI

ASANTE!
PIA NI WAKATI
WA KUONGEA
NA WENZANGU

BUMBUI ILIKUWA NA VIJIWE VYA KAHAWA, VILIVYOKUWA NA MIJADALA TOFAUTI
SANA, NA CHOPA ALIHESHIMIKA KATIKA KIJWE CHAKE.


MMM.
WANAWAKE KUONEWA,
MABINTI WA SHULE
KUBUGUZIWA?

NIMESIKIA
KUNAMWALIMU
ANAWAITA WANAFUNZI
WAKE "MCHUMBA" NA
KUWASHIKA-SHIKA

UNAONA!
MZEE KAOLINGA MBONA
HAMSEMI HAYA MAMBO.
MABINTI WANATESEKA
MJUE?




ALFAJIRI NYUMBANI KWA KINA SOFI. KABLA WAZAZI WAKE HAWAJA AMKA, ALIWAHI KUFANYA MIPANGO YA SIRI.



KWA VILE MAMA SOFI ALIKUWA AKIMFUATILIA NA KUMKAGUA SOFI KILA MUDA, AKIDHANI ATAJI DHURI. SOFI ALIGUNDTA MBINU MPPA.




WALIFIKA NYUMBANI KWA ZINJA PAKIWA PAMEPAMBAZUKA, ZINJA ALIKUWA NA SHAKU YA KUMKARIBISHA SOFI NYUMBANI KWAKE.




...WE USINISHIKE HIVO NILIKUOMBA UNISAIDIE! MIMI SIKO TAYARI KUFANYA HAYO UNAYOTAKA.

BEBI, KWENYE SHIDA MARAFIKI HUSAIDIANA, NISAIDE KWENYE HILI.




HAPANA. WEWE NI SITIRI TU, NIKIPATA NALLI NAONDOKA KWENDA KWA SHANGAZI. ILA MENGINE STAKI.



WE DEM FALA SANA, YAANI UNICHOMESHE MAFUTA NA MAHINDI KISA URAFIKI. TOKAAA

PUF!



ZINJAAAA NIACHEE!



YAANI TUMEMTAFUTA
KILA KONA HATUMWONI
MWENYEKITI.

ARGH,
ATAKUWA AMETOROKA.
KAOGOPA MILA. MABINTI
WA SIKU HIZI HAWANA
ADABU!.



MPAKA LEO BADO
MNAENDELEZA MAMBO
YA MILA!? MNASHANGAA
BINTI KUTOROKA?




SISI SIO WAZUNGU,
MBONA MNATAKA KUTUFANYA
WATUMWA. WAO WANAHUBIRI
MILA ZAO, NA SISI
TUNAFANYA ZETU?



UNAKOSEA!
UKEKETAJI NI HATARI
KWA MAISHA NA TUNAUPINGA
SANA! MUACHE MILA HIZI!
SASA TUMTAFUTE SOFI

TUMEELEWA!
HATUTAENDELEZA
MILA HIZI, TUTATAFUTA
ELIMU ZAIDI. KWASASA
TUSAIDIE NIMPATE
MWANANGU!



BAADA YA WAZAZI WA SOFI KUELEWA NA KUKUBALI
KUMTAFUTA SOFI, NDIPO SOFI ALIPOFIKA NYUMBANI
AKIWA ANALIA.

MAMA NISAMEHE,
MIMI NAOGOPA MILA
MNAZOPANGA KUNIFANYIA!
NIHURUMIENI!


MWANANGU...
JAMANI SOFIII WEWE!
NISAMEHE MIMI,
NA HATUTAFANYA
MILA HIZI ZA
UKEKETAJI WALA
KUKUOZESHA



WANAFUNZI WANGU!
NILIPOKEA MAONI KUHUSU
UONEVU NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA
HAPA SHULENI NA HUKO MTAANI.
KUANZIA LEO IWE MWISHO!
TUNAELEWANA!

NDIO
MWALIMU
MKUU!!

MBONA KAMA
KIMENUKA!
HATUBAKI
SALAMA LEO.



SAFI SANA!
KILIO CHETU KIMESIKIKA.
SASA TUTASOMA
KWA AMANI.

FAKI UTAPOKEA
BARUA TOKA KWA MWALIMU
WA NIDHAMU, UTAKUJIA
NA MZAZI WAKO!
WE MWALIMU WA ZAMU
NIFWATE

AMEYATIMBA.
MWADABISHE.
AMETUSUMBUA
SANA
DARASANI.



SIKUWA
NA DHAMIRA MBAYA YA
KUWADHALILISHA. NI.NI NANI...
MKUU NISAMEHE,
NIMEKOSA. TAFADHALI.

NINI? HAYO NI
MAKOSA YA MAKUSUDI
NAPELEKA SWALA HILI
KWENYE MKONO WA
SHERIA.



WASICHANA WANAPITIA
CHANGAMOTO NYINGI!
HAPA SHULENI PANATAKTWA
KILWA SEHEMU SALAMA KWAO!
SIWEZI KUSAMEHE TU!
SUBIRI TARATIBU ZA
NIDHAMU!

1. NI HATUA GANI ZINATAKIWA CHUKULIWA KUWAFANYA MABINTI KUSOMA KWA AMANI BILA BUGUDHA YEYOTE ILE, KWA MFANO: UKATILI WA KIJINSIA MASHULENI?

2. JE UNADHANI NI SAHIHI KWA WASICHANA WASIOFANYA VIZURI SHULENI KUOLEWA KATIKA UMRI MDOGO HATA KAMA WAMEAFIKI? ELEZEA.



3. UNAEZAJE KUWA NA UWEZO WA KUJIAMINI NA KUZUNGUMZA KUHUSU MATATIZO AU MASWAIBU YANAYOKUKUMBA SHULENI AU KWENYE JAMII YAKO?

KAMA JIBU LAKO NI NDIO AU HAPANA, TOA SABABU.

4. JE NI NANI UNAYEMWAMINI UNAEZA KUMWAMBIA/MSHIRIKISHA KUHUSU MATATIZO YAKO? ELEZEA.



Jarida hii maalum linachambua maswala muhimu la ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana, ikiwemo wale walio shuleni na wale nje ya mazingira ya shule. Jiunge nasi katika kuchochea mazungumzo, kuunda nafasi salama, na kutafuta jamii yenye haki na usawa zaidi.



Tai
Storytelling for Social Change



mundo cooperante